



TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 24 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 24 wa mwaka wa wanahisa wa Benki ya NMB utafanyika kwa njia ya mtandao siku ya Ijumaa tarehe 7 Juni, 2024 kuanzia saa 4 asubuhi. Ajenda itakuwa kama ifuatavyo:

- 24.1 MATANGAZO NA AKIDI
- 24.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
- 24.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 23 ULIOFANYIKA TAREHE 2 JUNI 2023
- 24.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 23 WA WANAHISA
- 24.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2023
- 24.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2023
- 24.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA VIWANGO VYA MALIPO YA WAKURUGENZI
- 24.8 KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI
- 24.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA 2024
- 24.10 MENGINEYO

MAELEZO MUHIMU

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria Mkutano lazima wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au Taarifa ya Akaunti (CSDR Account Statement).
2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi watakaohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kufuata/kuzingatia sheria na Katiba ya Kampuni. Fomu ya uwakilishi lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa Benki iliyopo Makao Makuu ya Benki ya NMB au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe Mwantumu.Salim@nmbbank.co.tz kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Alhamis tarehe 6 Juni 2024.
3. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria kikao watahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi (proxy forms) zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya Benki ya NMB (www.nmbbank.co.tz).
4. Wakurugenzi wamependekeza malipo ya gawio la shilingi 361.18 kwa kila hisa, ambayo ni jumla ya shilingi bilioni 180.59 kutokana na faida ya mwaka 2023.

Tarehe za kuzingatia:

Tarehe ya tangazo:	- 15 Mei 2024
Hisa kuuzwa pamoja na gawio :	- 15 Mei 2024
Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :	- 05 Juni 2024
Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:	- 06 Juni 2024 na kuendelea
Daftari la wanahisa kufungwa:	- 10 Juni 2024
Malipo ya gawio kwa wanahisa:	- 19 Juni 2024

Kwa agizo la Bodi.

Mwantumu Salim
Katibu wa Kampuni
15 Mei 2024